

Samaria

14 September 2014

John 4:1-26, 39-42

- I. Samaritan People, Samaritan Woman
 - A. North vs. South
 - B. Mutts and Purebreds (see Ezra 9-10)
 - C. Heretics and the Orthodox
 - D. A woman with a past

- II. Bridging the Divide
 - A. Jesus speaks to the woman
 - B. Jesus asks for water from the woman
 - C. Why? The gospel of God's grace. (see Luke 19:10)

- III. The Gift of God
 - A. The Gift (see John 3:3-6)
 - B. The Giver (see Numbers 20:1-13; 1 Corinthians 10:1-4)
 - C. The Recipient
 - D. Tasting the Living Water

- IV. The Desire of the Nations (vv. 25-26, 39-42)
 - A. The Teacher
 - B. The Savior of the World
 - C. What will you do?

Yohana (John) 4:1-26, 39-42

1 Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. 2 Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya, Tazama, namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako. 3 Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake. 4 Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. 5 Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao. 6 Na Yohana alikuwa amevaa singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, akala nziye na asali ya mwitu.

7 Akahubiri akisema, Yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuinama na kuilegeza gidamu ya viatu vyake. 8 Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu. 9 Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. 10 Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akishuka juu yake; 11 na sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe. 12 Mara Roho akamtoa aende nyikani. 13 Akawako huko jangwani siku arobaini, hali akijaribiwa na Shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia. 14 Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.

16 Naye alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya, akamwona Simoni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. 17 Yesu akawaambia, Njoni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. 18 Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. 19 Akaendelea mbele kidogo, akamwona Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, nao pia walikuwa chomboni, wakizitengeneza nyavu zao. 20 Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya chombo pamoja na watu wa mshahara, wakaenda, wakamfuata. 21 Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi, akafundisha. 22 Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi. 23 Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaza sauti, 24 akisema, Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuagamiza? 25 Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke. 26 Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka.

... 39 Akaenda akihubiri katika masinagogi yao, katika nchi yote ya Galilaya, na kutoa pepo. 40 Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, Ukitaka, waweza kunitakasa. 41 Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika. 42 Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika.